THE STATE EDUCATION DEPARTMENT /
THE UNIVERSITY OF THE STATE OF NEW YORK / ALBANY, NY 12234

Lissette Colon-Collins, Assistant Commissioner | Office of Bilingual Education and World Languages

55 Hanson Place, Room 594
Brooklyn, New York 11217
Tel: 718-722-2445 Fax: 718-722-2459

89 Washington Avenue, Room 528EB
Albany, New York 12234
Tel: 518-474-8775 Fax: 518-474-7948

SHERIA ZA HAKI ZA WAZAZI KWA WANAFUNZI WA LUGHA YA KIINGEREZA KATIKA JIMBO LA NEW YORK

Sheria za Kamishna wa Idara ya Elimu ya Jimbo la New York (NYSED) sehemu ya 154 inakupa wewe – mzazi/mlezi wa Wanafunzi wa Lugha ya Kiingereza (ELLs) –:

1. Haki ya watoto wako kupokea elimu ya umma bila malipo katika wilaya ya shule ambayo unaishi, haijalishi hali yako ya uhamiaji au ya watoto wako (k.m., kama wanafamilia wako ni raia, wahamiaji, au wasio halali) na lugha ambayo wewe au watoto wako wanaongea.

2. Haki ya kuwaandikisha watoto wako shuleni bila kuombwa kutoa maelezo au stakabadhi ambazo zinaweza kufichua hali ya uhamiaji ya watoto wako. Huwezi kuombwa utoe kadi au nambari ya ruzuku ya serikali, visa ya uhamiaji au hali ya visa, au stakabadhi za uraia au hali ya uraia.

3. Haki chini ya sheria ya serikali ya kuwa na mkalimani/mtafsiri kwa lugha yako unayopendelea kwa ajili ya mwingiliano muhimu na wilaya ya shule.

4. Haki ya kuwa na watoto wako katika mpango wa Elimu ya Lugha Mbili (Bilingual Education (BE)) wakati kuna wanafunzi 20 au zaidi wa kiwango cha gredi ambao wanaongea lugha moja ya nyumbani/msingi. [1]

5. Haki ya kupokea ilani iliyoandikwa kwa Kiingereza kwa lugha yako unayoipendelea kwamba watoto wako wametambuliwa kama ELL na watawekwa katika mpango wa Elimu ya Lugha Mbili au Kiingereza kama Lugha Mpya (iliyoitwa awali Kiingereza kama Lugha ya Pili). [2]

6. Haki ya kikao cha uelekezo cha ubora wa juu, kinachotolewa na wilaya ya shule yako, ambacho kinalenga viwango vya jimbo, mitihani, na matarajio ya shule ya ELL, na hata pia malengo na mahitaji ya mpango wa Elimu ya Lugha Mbili na Kiingereza kama Lugha Mpya. Uelekezo huu lazima ufanyike kabla ya mpango wa mwisho wa shule, na lazima uwe kwa lugha yako unayopendelea.

7. Haki ya kupokea maelezo kuhusu maendeleo ya lugha ya Kiingereza ya watoto wako, na hata pia kuhusu maendeleo ya lugha yao ya nyumbani ikiwa wako katika mpango wa Elimu ya Lugha Mbili.

8. Haki ya kukutana na wahudumu wa shule angalau mara moja kwa mwaka, kwa kuongezea mikutano mingine ya jumla inayohitajika, ili kujadili maendeleo ya jumla ya masomo na lugha ya watoto wako.

9. Haki ya watoto wako kuwekwa katika mpango wa Elimu ya Lugha Mbili au Kiingereza kama Lugha Mpya katika siku 10 baada ya kuandikishwa, na haki ya kutoka kwenye mpango wa Elimu ya Lugha Mbili. Kwa kiwango cha chini, lazima watoto wako wapokee Kiingereza kama maagizo ya Lugha Mpya.

10. Haki ya watoto wako kuhamia shule nyingine katika waliya yako ambayo inatoa Elimu ya Lugha Mbili kwa lugha yako, kama shule ya asili ya watoto wako haitoi mpango kama huo.

11. Haki ya watoto wako kuwa na nafasi sawa za mipango na huduma zote zinazotolewa na wilaya ya shule, zinazofaa umri na kiwango cha gredi ikiwa ni pamoja na zinazohitajika ili kuhitimu, na kwa mipango yote ya shule inayohitajika kwa wanafunzi wengine.

12. Haki ya watoto wote kupokea maagizo yote muhimu ya mtalaa, na kujifunza Kiingereza na masomo mengine kama vile Sanaa ya Kusoma/Lugha, Hesabu, Sayansi, na Masomo ya Jamii katika kiwango kimoja cha kitaaluma kama watoto wale wengine wote. Kuwa na haki za huduma za ELL hakuzuii uwezo wa kupata maagizo muhimu ya mtalaa.

13. Haki ya watoto wako kuhusika vikamilifu katika shughuli za ziada (vilabu vya baada ya shule, michezo, n.k.). Kuwa na haki za huduma za ELL hakuzuii uwezo wa kushiriki katika shughuli za ziada.

14. Haki ya watoto wako kupata huduma za usaidizi (k.m., Huduma za Kuingilia kati Kitaaluma) zinazolingana na mipango yoyote ya uingiliaji kati ambayo shule/wilaya inatoa kwa wanafunzi wote.

15. Haki ya watoto wako kufanya mitihani kila mwaka ili kubainisha maendeleo yao ya lugha ya Kiingereza, na kupata maelezo kuhusu utendakazi wa watoto wako katika mitihani hiyo ya kitaaluma, ikiwa ni pamoja na mitihani ya Jimbo la New York.

16. Haki ya watoto wako kuendelea kuandikishwa kila mwaka katika mpango wa Elimu ya Lugha Mbili au Kiingereza kama Lugha Mpya wakiwa bado katika ELL.

17. Haki ya Kuwasiliana na Ofisi ya Idara ya Elimu ya Jimbo la New york ya Elimu ya Lugha Mbili na World Languages ikiwa haki zozote hapa juu zimekiukwa.

    Tafadhali piga simu kwa **ELL Parent Hotline** nambari ya simu **1-800-469-8224**, au tuma barua pepe kwa: nysparenthotline@nyu.edu

    Kwa maelezo zaidi, tembelea: **www.p12.nysed.gov/biling**
    au andika barua kwa:

    New York State Education Department
    Office of Bilingual Education & World Languages
    55 Hanson Place, Room 594
    Brooklyn, New York 11217

[1] Katika Jiji la New York, kulingana na Amri ya Kibali cha Aspira, mpango wa BE unahitajika katika gredi K-8 kama wanafunzi 15 au zaidi wa kiwango cha gredi wanaongea lugha moja katika gredi mbili zinazotangamana. Ikiwa kuna idadi ya kutosha ya wanafunzi wanaofaa katika shule, lakini wako katika wilaya ya shule, lazima wilaya itoe mpango wa BE.

[2] ELL zote hukuza ujuzi wake wa Kiingereza kupitia kozi za “Kiingereza kama Lugha Mpya”. Kwa kuongezea, wale walio katika mpango wa Elimu ya Lugha Mbili hufanya pia Sanaa ya Lugha ya Nyumbani. Kozi muhimu za mtalaa (k.m., Hesabu, Sayansi, na Masomo ya Kijamii) hutolewa katika mpango wa Elimu ya Lugha Mbili kwa Kiingereza na lugha yao ya nyumbani. Wale ambao hawako katika mpango wa Elimu ya Lugha Mbili hufanya kozi muhimu za mtalaa *kwa Kiingereza*.